

**MKATABA WA KUPANGISHA ENEO**

**BAINA YA**

**KAMPUNI YA KITULWE COMPANY LIMITED**

**NA**

**ATHUMANI RAMADHANI MANDIA**

**MKATABA WA KUPANGISHA ENEO BAINA YA KAMPUNI YA KITULWE  
COMPANY LIMITED NA ATHUMANI RAMADHANI MANDIA**

Mkataba huu ni baina ya kampuni ya **KITULWE COMPANY LIMITED** ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama mpangaji na Bwana **ATHUMANI RAMADHANI MANDIA** ambaye katika mkataba huu atajulikana kama mwenye eneo (Mpangishaji).

Mpangaji amekubali kupanga eneo lenye ukubwa wa ekari 20 lililopo katika Kijiji cha **Kwasemgaya**, Wilaya ya **Muheza** mkoa wa **Tanga** kwa makubaliano haya yafuatayo:-

1. Mkataba huu unahusu ekari 20 zinazomilikiwa na mpangishaji;
2. Eneo linalopangishwa linamilikiwa kihalali na mpangishaji lipo Kijiji cha **Kwasemgaya**, Wilaya ya **Muheza** mkoa wa **Tanga**;
3. Eneo la **Kwasemgaya** ni eneo lilipo kijijini na halina hati;
4. Mkataba huu utanzia leo Tarehe **14 Mwezi Septemba Mwaka 2021** hadi Tarehe **14 Mwezi wa Septemba Mwaka 2025**;
5. Mpangaji atalipa kodi ya pango Shilingi za Kitanzania 4,000,000/ kwa mwaka kwa kwa maneno **Shilingi** za Kitanzania **milioni nne** kwa mwaka kwa mkupuo mmoja wakati wa kusaini Mkataba;
6. Mpangishaji akishapokea fedha atakabidhi eneo hilo mara moja kwa Mpangaji;
7. Gharama za kodi zinaweza kubadilika katika kipindi cha miaka mitatu (3) kwa Mpangaji kupewa taarifa na Mpangishaji ndani ya kipindi kisichopungua miezi mitatu (3);
8. Kodi iliyokwishalipwa hairudishwi endapo Mpangaji atavunja Mkataba mwenyewe;

9. Mpangaji haruhusiwi kupangisha eneo alilopanga au kumwachia mtu mwingine wakati wa mkataba wake bila ruhusa ya mpangishaji;
10. Mpangaji atatakiwa kutunza mazingira ya eneo na vitu vyote kwa wakati mmoja (usafi);
11. Mpangaji anaruhusiwa kufanya shughuli yeyote ya kibiashara katika eneo alilopanga ili mradi havunji sheria za nchi;
12. Ifikapo mwisho wa mkataba mpangaji atakabidhi eneo alilopanga bila masharti yeyote na iwapo kuna mali za mpangaji basi mpangaji anaruhusiwa kuondoka nazo;
13. Kama Mpangaji ataendelea na mkataba mpya baada ya **14 Mwezi wa Septemba Mwaka 2025** atamjulisha mpangishaji na kama haendelei pia utamjulisha mpangishaji ndani ya miezi mitatu (3) kabla ya kipindi chake cha Mkataba kwisha.
14. Kwa kuthibitisha mkataba huu kwa pande zote zinaweka sahihi zao kwa makubaliano yote yaliyoandikwa kwenye mkataba kwa hiari yao.

**Jina na Sahihi Mpangishaji:**

**ATHUMANI RAMADHANI MANDIA** Sahihi .... *Athumani* ..... 14 Septemba 2021

**Jina na Sahihi Mpangaji:**

**KITULWE COMPANY LIMITED** Sahihi ..... *[Signature]* ..... 14 Septemba 2021



**Jina na Sahihi Shahidi:**

**FINIAS LADSLAUS KINIGWA** Sahihi ..... *[Signature]* ..... 14 Septemba 2021

